# MUHTASARI WA TAARIFA - ROBO YA KWANZA, 2024

## Utangulizi:

Kuelekea mwishoni mwa robo ya kwanza ya mwaka, Mawaziri wa afya kutoka nchi zenye athari ya maambukizi makubwa ya malaria (HBHI), walikutana Yaunde nchini Kameruni, na kutoa dhamira ya kuchukua hatua za haraka katika mapambano kuelekea kutokomeza vifo vinavyotokana na malaria kwa kuimarisha mbinu za namna ya kushughulikia nchi zenye athari ya maambukizi makubwa ya malaria (HBHI). Ahadi hiyo imeelezwa katika *Tamko la Yaunde.*

## Nguzo Nne Muhimu:

Mawaziri wanathamini na kukubali kuwa nguzo nne za HBHI ni muhimu sana katika kukabiliana na ugonjwa wa malaria kwa uendelevu na usawa ili kudhibiti kwa ufanisi na hatimae kutokomeza malaria. Nguzo hizo muhimu ni;

1. Utashi wa kisiasa (katika ngazi zote),
2. Matumizi ya kimkakati ya taarifa katika utekelezaji,
3. Mwongozo bora wa kiufundi,
4. Uratibu wenye ufanisi.


Mawaziri pia wanathamini kuwa nguzo hizi nne, haziwezi kufanya kazi katika ombwe, bali inahitaji uwepo wa mfumo wa afya wa kitaifa ambao umekubalika na unaofanya kazi vizuri ukilenga mtazamo wa kushirikisha sekta mbalimbali, taasisi za umma pamoja na sekta binafsi. Sekretarieti ya ALMA ipo tayari kujitolea kusaidia nchi na wadau katika kutekeleza dhamira hii ya mawaziri.

## Kuimarisha Ahadi za Kisiasa:

Ili kuunga mkono ahadi ya mawaziri juu ya kuhamasisha uongozi katika sekta mbalimbali, ALMA imejitolea kuhamasisha nchi wanachama ili waweze kuunda mabaraza ya kutokomeza malaria, ambayo yanajumuisha viongozi kutoka sekta mbalimbali serikalini, viongozi wa kimila, viongozi wa dini, viongozi toka sekta binafsi, asasi za kijamii na viongozi wa makundi ya vijana.


WANACHAMA
Algeria
Angola
Benin
Botswana
Burkina Faso
Burundi
Cameroon
Central African Republic
Cabo Verde
Chad
Comoros
Republic of Congo
Côte d'Ivoire
Democratic Republic of Congo
Djibouti
Egypt
Equatorial Guinea
Eritrea
Eswatini
Ethiopia
Gabon
Ghana
Guinea
Guinea Bissau
Kenya
Lesotho
Liberia
Libya
Madagascar
Malawi
Mali
Mauritania
Mauritius
Mozambique
Morocco
Namibia
Niger
Nigeria
Rwanda
Sahrawi Arab Democratic Republic
São Tomé and Príncipe
Senegal
Seychelles
Sierra Leone
Somalia
South Africa
South Sudan
Sudan
The Gambia
Togo
Tunisia
Uganda
United Republic of Tanzania
Zambia
Zimbabwe

**Uzinduzi wa Mabaraza ya Malaria na Magonjwa Yasiyopewa Kipaumbele.**




**Chanzo: Robo 1 2024 - Kadi ya Alama ya Ufuatiliaji na Uwajibikaji**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria, mipaka yake na mamlaka ya nchi yeyote.*

**Asilimia ya Mipango Mikakati ya Malaria iliyopata ufadhili kwa kipindi (2024-2026)**




**Chanzo: Robo 1, 2024 - Kadi ya Alama ya Ufuatiliaji na Uwajibikaji**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria, mipaka yake na mamlaka ya nchi yeyote.*

Hadi sasa, ni nchi nne tu kati ya zilizo na athari ya maambukizi makubwa ya Malaria, ambazo tayari zimeshaunda mabaraza ya kutokomeza malaria. Nchi hizo ni Msumbiji, Tanzania, Uganda na Nigeria, kukiwa na uwezekano mkubwa wa kushirikisha viongozi wengine ili kuhamasisha kupata rasilimali zaidi kwa ajili ya utekelezaji wa programu za kitaifa za kudhibiti malaria.

Nchi mbili zenye athari kubwa ya maambukizi ya malaria; Kameruni na Burkina Faso zipo katika mchakato wa kuanzisha mabaraza ya kutokomeza malaria, wakati nchi 5 zilizobakia; Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo, Ghana, Mali, Niger na Sudan wanapaswa kuanzisha bodi za ngazi za juu zenye wajibu wa kutokomeza malaria.


Mawaziri wote wanahimizwa kuridhia *Tamko la Yaunde* lililopitishwa na Wakuu wa nchi na serikali, ili kuhakikisha uwepo wa dira ya taifa, mpango wa maendeleo na kutenga bajeti ili kutoa kipaumbele katika kutokomeza malaria. Hadi sasa, ni nchi moja tu kati ya zote zenye athari ya maambukizi makubwa ya Malaria, ambayo asilimia 80 ya bajeti yake ya kudhibiti malaria imepata ufadhili.

**Uongozi katika kusimamia programu za malaria na mifumo mingine ya programu za afya:**

Uimara na uthabiti wa mifumo ya afya, utaamua kwa kiasi kikubwa mafanikio ya udhibiti na kutokomeza malaria. Hii inajumuisha ushirikiano kati ya programu za afya, sekta zingine za serikali pamoja na sekta binafsi.

Nchi wanachama na wadau wamekubaliana kupitisha muundo wa kina na kupeleka rasilimali kwenye maeneo ya utekelezaji ngazi za chini, ili kuleta ufanisi na mafanikio makubwa zaidi.


**Kupungua kwa visa vipya vya malaria kwa angalau asilimia 75 ifikapo 2025 (ukilinganisha na mwaka 2015)**



Lengo limefikiwa / utekelezaji unaendelea vizuri
Juhudi zaidi zinahitajika kufikia lengo
Utekelezaji upo nje ya lengo
Hamna Takwimu/ Haihusiki

**Chanzo: Robo 1 2024 - Kadi ya Alama ya Ufuatiliaji na Uwajibikaji**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria, mipaka yake na mamlaka ya nchi yeyote.*

**Asilimia ya Ugawaji wa Dawa kufikia Malengo ya Shirika la Afya Duniani**




Lengo limefikiwa / utekelezaji unaendelea vizuri
Juhudi zaidi zinahitajika kufikia lengo
Utekelezaji upo nje ya lengo
Hamna Takwimu/ Haihusiki


**Chanzo: Robo 1 2024 - Kadi ya Alama ya Ufuatiliaji na Uwajibikaji**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria, mipaka yake na mamlaka ya nchi yeyote.*

Kwa sasa, Ghana ndio nchi pekee kati ya zilizo na athari ya maambukizi makubwa ya malaria ambayo imefikia lengo na inaendelea kupunguza visa vipya vya malaria. Hata hivyo, hali ya utekelezaji kuhusiana na magonjwa yasiyopewa kipaumbele haiko vizuri, ambapo ingeweza kujumuishwa katika programu ya udhibiti wa malaria, kwa kuwa programu hizi mbili pamoja na ugawaji wa bidhaa vinapaswa kutolewa na wahudumu wa afya ngazi ya jamii. Kuhusiana na magonjwa ambayo yalikuwa hayapewi kipaumbele, Tanzania, Uganda na Mali, ndizo ambazo zimeweza kufikia malengo ya Shirika la Afya Duniani, kati ya nchi zilizo na athari ya maambukizi makubwa ya malaria.

**Uhamasishaji katika ngazi zote ili kuimarisha uongozi na rasilimali:**


Kuna fursa kwa sekta zote kuainisha majukumu yao na kuchangia katika kuimarisha mifumo, udhibiti na kuzuia mbu, na kujumuisha mikakati ya kudhibiti malaria katika sera, programu, na kutenga fedha katika bajeti zao.

**Kusaini, kuridhia na kuwasilisha utekelezaji wa AMA kwa Kamati ya Umoja wa Afrika.**




**Chanzo: Robo ya 1 2024 - Kadi ya Alama ya Ufuatiliaji na Uwajibikaji**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria, mipaka yake na mamlaka ya nchi yeyote.*

**Shughuli za Malaria zilizo katika Mpango Mkakati wa Malaria zinazowalenga Wakimbizi**





**Chanzo: Robo ya 1 2024 - Kadi ya Alama ya Ufuatiliaji na Uwajibikaji**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria, mipaka yake na mamlaka ya nchi yeyote.*

Mamlaka huru za udhibiti za kitaifa kwa kushirikiana na Wizara za Mambo ya nje, wanapaswa kuunga mkono kuidhinishwa kwa sheria iliyotungwa kuhusu Mamlaka ya Dawa ya Afrika, ili kuhakikisha nchi wanachama zinanufaika kutokana na kuboresha upatikanaji wa dawa na uwepo wa juhudi za pamoja zilizoainishwa na kuratibiwa, ili kuwezesha viwanda vya ndani kutengeneza bidhaa za kimatibabu. Wizara zinazoshughulikia mambo ya ndani na mambo ya nje zinaweza kushiriki juhudi za kutoa huduma kwa wakimbizi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya.

Baraza la kutokomeza Malaria na Magonjwa yasiyopewa kipaumbele, yanatakiwa kuanzisha mfuko ili kupata rasilimali fedha toka sekta binafsi, kufanya kazi pamoja na programu za malaria; matumizi ya kadi ya alama ya ufuatiliaji na uwajibikaji ngazi ya taifa na ngazi za chini, ili kufuatilia maendeleo, kutambua vikwazo na changamoto zinazohitaji kufanyiwa kazi.

**Nchi zilizodhibiti /Kutokomeza Malaria zilizo na Kadi ya Alama ya Ufuatiliaji na Uwajibikaji**



**Chanzo: Robo 1 2024 ALMA Kadi ya Alama ya Ufuatiliaji na Uwajibikaji**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria, mipaka yake na mamlaka ya nchi yeyote.*

Mawaziri wametambua kuwa upungufu mkubwa wa fedha umezuia juhudi za kupambana na malaria ipasavyo, na hivyo ni muhimu kuimarisha upatikanaji wa rasilimali toka vyanzo vya ndani; sekta za umma na binafsi. ALMA itafanya kazi na serikali kuhakikisha kuwa kadi za alama ya ufuatiliaji na uwajibikaji za nchi, zinazingatia viashiria muhimu vya kufanikisha ahadi kama ilivyo katika *Tamko la Yaunde.*

**Kuhakikisha Mkakati wa Matumizi ya Taarifa kwa ajili ya utekelezaji:**

Mawaziri wameahidi kuwekeza katika mifumo ya taarifa za afya zenye ufanisi na uhakika, ikijumuisha uchambuzi na teknolojia ya mfumo wa habari wa kijiografia. Wameahidi kuimarisha matumizi ya mifumo hii ili kusaidia kutambua ukubwa, utabaka na mtawanyo wa hatari ya maambukizi ya malaria, viashiria muhimu vya afya, na kulenga utekelezaji wa afua mbalimbali, ili kupata matokeo mazuri.

ALMA imejitolea kuzisaidia nchi kubuni zana zinazofaa katika kufuatilia na kuripoti takwimu kwa ajili ya kufuatilia matokeo kwa kila nchi wanachama. Hii itarahisisha kurekebisha uwekezaji uliofanyika katika kutekeleza afua na mikakati mbalimbali, ili kupata matokeo kutokana na kiwango cha athari ya malaria katika maeneo husika.

Kuhamasisha na kuhimiza kujifunza kwa njia ya kielektroniki, na kujitoa katika kuwaunga mkono Mawaziri kutumia teknolojia zinazofaa, na kuhakikisha mafunzo yanakuwa ni ya gharama nafuu; ALMA imejitolea kuanzisha moduli za mafunzo zilizokubaliwa kuhusu kadi ya alama ya ufuatiliaji na uwajibikaji katika jukwaa maalum la kujifunza.

Kurekebisha na kukubaliana juu ya zana za kadi ya alama ya ufuatiliaji na uwajibikaji, kuwiana na kila nchi ili kufuatilia ngazi zote; mikoa, wilaya hadi ngazi ya jamii, pamoja na zana ya uwajibikaji katika usimamizi na ufuatiliaji wa programu mbalimbali za afya na wafanyakazi, ili kuboresha huduma inayotolewa ikijumuisha huduma ya kinga, utambuzi na matibabu ya malaria.

**Umoja wa Afrika na Kamati ya Uchumi ya Kikanda:**

ALMA ina mkataba wa makubaliano na Kamati ya Umoja wa Afrika; Umoja wa wadau wanaoshughulika na harakati za kutokomeza malaria, na vitalu vya kiuchumu. *Tamko la Yaunde* litafanyiwa kazi kwa ushiriki wa kikanda, kuhakikisha msaada kwa ajili ya kuimarisha ufuatiliaji na uwajibikaji hadi ngazi za chini, ushirikiano thabiti wa maeneo ya mipakani pamoja na uangalizi mzuri wa kisiasa wa kikanda.

**HITIMISHO:**

Mapambano dhidi ya malaria barani Afrika, ni dhima ya sekta na wadau mbalimbali; umuhimu kwa ukuaji wa jumla na maendeleo ya bara zima la Afrika. Kwa nchi zilizo na athari ya maambukizi makubwa ya Malaria, inarudisha nyuma maendeleo ya kiakili, kujifunza, kupunguza umaskini, tija, ukuaji na ajira kwa sehemu kubwa ya jamii.

*Tamko la Yaunde*, ni fursa kwa wadau na washirika kwa kila nchi kuungana na kuratibu utaalamu wa pamoja na uwezo wa kumaliza vifo vinavyotokana na malaria.

***Ziro malaria inaanza na mimi; Inaanza na sisi sote.***